

102/3
KISWAHILI
Karatasi ya 3
FASIHI
Julai 2018
Muda: Saa 2 ½

MTIHANI WA PAMOJA WA NYANDARUA MAGHARIBI

KIDATO CHA NNE

KISWAHILI

Karatasi ya 3

FASIHI

Maagizo

- (a) Jibu maswali **manne** pekee.
- (b) Swali la **kwanza** ni la **lazima**.
- (c) Maswali hayo mengine **matatu** yachaguliwe kutoka sehemu **nne** zilizobaki..
- (d) Usijibu maswali **mawili** kutoka **sehemu moja**.
- (e) Majibu yote **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.
- (f) Karatasi hii ina kurasa 4 zilizopigwa chapa.
- (g) Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

SEHEMU YA A: USHAIRI

Lazima

Soma shairi ulilopewa kwa makini kisha ujibu maswali

Mwenye macho wafishasha, wajiona kama ndovu
Kitu kimekuleweshwa, huutambuwi uovu,
Ngoma yako itakesha, au ni nguvu za povu.
Tangu lini muwerevu, akajinyowa mwenyewe?

Tangu ukipate kitu, 'megeuka mpumbavu,
Kau hutuamini mtu, ambaye kwamba mtovu,
Wafikiri kisu gutu, hakikati nyama pevu?
Tangu lini muwerevu, akajinyowa mwenyewe?

Wangapi meonekana, mibakhili mishupavu,
Waliyo wakijitona, na wingi usuluhivu,
Leo hawanasi tena, wage ukila maivu.
Tangu lini muwerevu, akajinyowa mwenyewe?

Kupata kusikughuri, ukajidhani mwerevu,
Wa hicho chako kiburi, wewe ni maangavu,
Iko siku itajiri, ujikute kwenye wavu
Tangu lini muwerevu, akajinyowa mwenyewe?

Kila mwenye kukuonya, uiwate ndiya mbovu,
Huchelewi kumuvinya, kumvunda zake mbavu,
Fanya ambayo wafanya, hutajinyowa mashavu,
Tangu lini muwerevu, akajinyowa mwenyewe?

Maswali ya shairi.

- (a) Lipe shairi hili kichwa mwafaka. (alama 1)
- (b) Fafanua toni ya mwandishi. (alama 2)
- (c) Eleza dhamira katika shairi hili. (alama 2)
- (d) Pambanua umbo la ubeti watatu. (alama 3)
- (e) Dhihirisha tamathali ya usemi iliyotumiwa katika mloto wa ubeti wa pili. (alama 2)
- (f) Kwa kutoa mifano , onyesha mbinu ambazo mwandishi ametumia kufanikisha kazi yakekiarudhi. (alama 4)
- (g) Uandike ubeti wa nne kwa lugha ya nathari. (alama 4)
- (g) Eleza maana za maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi. (alama 2)
 - (i) Kitu
 - (ii) Mtovu

SEHEMU B: RIWAYA

Ken Walibora: Kidagaa Kimemwozea

Jibu swali la 2 au la 3.

2.”Haki nakwambia ...afadhali mkoloni mzungu kuliko mkoloni mweusi....huyu mweusi ...anatumia wenzake kama kopo la msalani.”

- a) Eleza muktadha wa dondoo hli. (alama 4)
 - b) Bainisha tamathali mbili za usemi zilizotumiwa kwenye dondoo. (alama 4)
 - c) Kwa kurejelea riwaya nzima,thibitisha kuwa mkoloni mweusi anawatumia wenzake kama kopo la msalani. (alama 12)
- .
3. Fafanua ujumbe wa mwandishi kupitia kwa mbinu zifuatazo. (Alama 20)
- a) Barua
 - b) Mashairi.

SEHEMU C: TAMTHILIA

Kigogo.Pauline Kea.

Jibu swali la 4 au la 5.

4. “Nafikiri inayokuhikumu ni nafsi yako”
- a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
 - b) Jadili mambo yoyote **kumi** ambayo msemewa anajihukumu kwayo. (alama 10)
 - c) Jadili mambo wanayoyafanya wanasagamoyo ili kujikomboa kutokana na changamoto zinazowakuba. (alama.6)
5. Jadili matumizi ya mbinu ya majazi kwa kurejelea, (alama 20)
- i) Majoka
 - ii) Tunu

SEHEMU D: HADITHI FUPI

Alifa Chokocho na Dumu Kayanda Tumbo Lisiloshiha

6. Kwa kurejelea hadithi zozote, jadili changamoto zinazokuba asasi ya ndoa na familia.
(ala.20)

SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

7. (a) Lulu, Mwanangu tulia,
Wewe mtoto lala, mvua imekuja
Si uwongo hata na miti hulichagnamkia.
Hakuna haja ya kuelezwa.
Lulu mvana tulia.
- (a) (i) Bainisha kipera cha utungo huu. (alama 2)
(ii) Toa sababu tatu za jawabu lako. (alama 3)
(iii) Bainisha mambo yoyote matano yanayoweza kufanikisha uwasilishaji wa utungo huu. (alama.5)
- (b) Tofautisha kati ya vitendawili na methali. (ala.10)

HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWACHAPA